Majibu

A. KUSIKILIZA NA KUZUNGUMZA (QR 1 – Ukurasa wa 42)

1. Kusikiliza na kujibu

a. Kusikiliza na kujibu mazungumzo ya kawaida

Jitathmini 1.1 (ukurasa wa 1)

1. Kusikiliza na kujibu mazungumzo ya kawaida kunahusu kupokea maneno au ujumbe unaopitishwa na kuitikia kuonyesha umeelewa ujumbe.
2. (a) Nyanya na wajukuu wanasemezana, wanaota moto wakiendelea kusemezana, wanazungumzia mambo yanayowaathiri katika hali ya kawaida kama vile kubaleghe na usafi wa kibinafsi na pia wanazungumza ana kwa ana.
(b) Anakuwa makini na anamtazama Nyanya anapozungumza.
(c) Alikuwa akichochea moto Nyanya alipouliza swali.
(d) Kusikiliza kwa makini, kumwangalia anayezungumza ana kwa ana na kuepuka vizuizi vya mawasiliano kwa vile alikuwa akichochea moto Nyanya alipokuwa akizungumza.
(e) Kwa sababu mbwa anabweka na kumfanya Nyanya asisikie hoja ya mwisho ya Tina.
3. (a) Maria yuko makini, Maria anamtazama Nyanya kwa makini, Maria na Tina wanaepuka vizuizi vya mawasiliano, kumtazama Nyanya ana kwa ana na hakuna ambaye amekata kauli ya mwingine.
(b) kumtazama mzungumzaji kwa makini na kuepuka vizuizi kwa vile Boke anachochea moto Nyanya anapouliza swali.
4. (a) Lugha ya adabu imetumika, kila mmoja amesubiri zamu yake ya kuzungumza ifike, kila mmoja amejibu kwa kuzingatia kiini cha swali, lugha inayoeleweka imetumika, sauti inayosikika imetumika na wamejibu kwa ukakamavu na ujasiri.
(b) Rejelea sehemu ya **Kumbuka** katika ukurasa wa 2.
5. (a) Rejelea vipengele vya kuzingatia katika kusikiliza mazungumzo ya kawaida vilivyo kwenye sehemu ya **Kumbuka** katika ukurasa wa 2.
(b) Rejelea vipengele vya kuzingatia katika kujibu mazungumzo ya kawaida vilivyo kwenye sehemu ya **Kumbuka** katika ukurasa wa 2.
6. Unaweza kutumia kipakatalishi, simu, tabuleti au kompyuta kufanya zoezi hili. Tafiti tu kwenye mtandao salama ili ufanye mazoezi uliyopewa.
7. Mnapoigiza, zingatia vipengele vya kusikiliza na kujibu mazungumzo ya kawaida mlivyojifunza.
8. Fanya zoezi hili ukiwa na mzazi au mlezi wako. Hakikisha umezingatia vipengele vya kusikiliza na kujibu mazungumzo ya kawaida ulivyojifunza.

b. Kusikiliza na kujibu mahojiano

Jitathmini 1.2 (ukurasa wa 3-4)

1. (a) Aamba anauliza maswali halafu Guyo anayajibu.
(b) Anajibu maswali inavyofaa na anatumia ishara kama vile kutikisa kichwa kuonyesha kuwa amesikia swali.
(c) kutikisa kichwa
(d) karibu sana, asante, nimeshukuru

(e) Huonyesha heshima, kunakuwezesha kusikia kile anachokisema mzungumzaji na pia unampa fursa ya kukamilisha wazo lake.
2. (a) Kusikiliza kwa makini, kuepuka vizuizi vya mawasiliano, kutumia viziada lugha (kutikisa kichwa) na kutomkata mzungumzaji kauli.
(b) Rejelea sehemu ya **Kumbuka** katika ukurasa wa 3-4 kupata vipengele zaidi vya kusikiliza mahojiano.
3. (a) Kutumia lugha ya adabu, kutokata kauli, kujibu kwa kuzingatia kinachoulizwa na kuepuka hisia kali.
(b) Rejelea sehemu ya **Kumbuka** katika ukurasa wa 4 kupata vipengele zaidi vya kujibu mahojiano.
4. (a) Hakiki hoja zako kwa kurejelea vipengele vya kusikiliza mahojiano vilivyo katika sehemu ya **Kumbuka** katika ukurasa wa 3-4.
(b) Hakiki hoja zako kwa kurejelea vipengele vya kujibu mahojiano vilivyo katika sehemu ya **Kumbuka** katika ukurasa wa 4.
5. Unaweza kutumia kipakatalishi, simu, tabuleti au kompyuta kufanya zoezi hili. Tafiti tu kwenye mtandao salama ili ufanye mazoezi uliyopewa.
6. Mnaposhiriki mahojiano, zingatia vipengele vya kusikiliza na kujibu mahojiano mlivyojifunza.
7. Fanya zoezi hili ukiwa na mzazi au mlezi wako. Hakikisha umezingatia vipengele vya kusikiliza na kujibu mahojiano ulivyojifunza.

c. Kusikiliza na kujibu mjadala

Jitathmini 1.3 (ukurasa wa 4-5)

1. (a) Kuna mada inayojadiliwa na kuna pande mbili ambapo upande mmoja unatetea mada ilhali upande mwingine unapinga mada hiyo.
(b) Wanatoa hoja zinazoafiki upande wa mjadala wanaoegemea.
(c) Ili kutoa hoja zinazoafiki upande wa mada ambao umeamua kuegemea.
(d)

- Utohozi – teknolojia, mashine
- Taswira – mitambo ambayo inaweza kuzoa uchafu na kuusafirisha
- Nahau – tutilie maanani
- Msemo – pesa chungu nzima
- Uradidi – mara kwa mara
- Swali la balagha – Je, mmewazia suala la watu kupoteza ajira kutokana na matumizi ya mashine hizo?

(e) Ametumia swali la balagha na pia ametoa maelezo ya kina yanayoambatana na mfano.
(f) karibuni, asante sana, ninaomba, asante kwa kunipa fursa hii na asanteni sana
2. (a) Kusikiliza kwa makini, kumtazama anayezungumza ana kwa ana, kuepuka vizuizi vya mawasiliano na kutomdhalilisha mzungumzaji.
(b) Hakiki hoja zako kwa kurejelea vipengele vya kuzingatia katika kusikiliza mahojiano vilivyo katika sehemu ya **Kumbuka** katika ukurasa wa 5.
3. (a) Kuchangia zamu yako inapofika, kutumia lugha ya adabu na heshima, kuzingatia ukweli wa mada, kutumia mbinu mbalimbali za lugha na kutumia lugha rahisi.

(b) Hakiki hoja zako kwa kurejelea vipengele vya kuzingatia katika kuchangia mjadala vilivyo katika sehemu ya **Kumbuka** katika ukurasa wa 5.
4. (a) Hakiki hoja zako kwa kurejelea vipengele vya kuzingatia katika kusikiliza mjadala vilivyo kwenye sehemu ya **Kumbuka** katika ukurasa wa 5.
(b) Hakiki hoja zako kwa kurejelea vipengele vya kuzingatia katika kuchangia mjadala vilivyo kwenye sehemu ya **Kumbuka** katika ukurasa wa 5.
5. Unaweza kutumia kipakatalishi, simu, tabuleti au kompyuta kufanya zoezi hili. Tafiti tu kwenye mtandao salama ili ufanye mazoezi uliyopewa.
6. Mnaposhiriki mjadala, zingatia vipengele vya kusikiliza na kuchangia mjadala mlivyojifunza.
7. Fanya zoezi hili ukiwa na mzazi au mlezi wako. Hakikisha umezingatia vipengele vya kusikiliza na kuchangia mjadala ulivyojifunza.

d. Kusikiliza habari na kujibu
Jitathmini 1.4 (ukurasa wa 6)

1.
- Kusikiliza kwa makini wazo kuu.
- Kutambua maneno muhimu yanayorudiwa.
- Kuangalia vidokezo au mifano inayotolewa na mzungumzaji.

2. (a)
    - Ufafanuzi wa maadili ya mtu binafsi kama vile ukweli, nidhamu na uchapakazi.
    - Umuhimu wa maadili katika kujenga uhusiano mwema.
    - Athari za ukosefu wa maadili kama vile migogoro na chuki.

(b)
- Maadili
- Waadilifu
- Mshikamano

(c)
- Maadili: Mienendo na tabia njema zinazomwongoza mtu maishani.
- Waadilifu: Watu wenye tabia njema na waaminifu.
- Mshikamano: Hali ya watu kuungana na kufanya kazi pamoja kwa amani.

(d)
- Maadili huleta amani na upendo
- Ukosefu wa maadili huleta chuki na migogoro
- Kila mtu anapaswa kuwa na maadili ili kujenga jamii bora.

3. Rejelea majibu ya nambari ya 1 ili yakuelekeze kufanya shughuli hii.
4. Unaweza kutumia kipakatalishi, simu, tabuleti au kompyuta kufanya zoezi hili. Tafiti tu kwenye mtandao salama ili ufanye mazoezi uliyopewa.
5. Fanya zoezi hili ukiwa na mzazi au mlezi wako. Hakikisha unazingatia vipengele vinavyokuelekeza kufasiri suala muhimu katika habari ulivyojifunza.

i. Usikilizaji husishi
Jitathmini 1.5 (ukurasa wa 6-7)

1. Usikilizaji husishi unahusu msikilizaji kushiriki kikamilifu katika mazungumzo kwa kuonyesha umakini, kuuliza maswali ya ufafanuzi na kutumia ishara za mwili kuonyesha uelewa.

2. (a) Kunyosha mkono, kusikiliza kwa makini, kutumia ishara za mwili.
(b) Faraja ananyosha mkono na kuomba ufafanuzi ("Alimaanisha nini...?"), Pendo anamsikiliza kwa makini na kumjibu kwa utaratibu na Faraja anatikisa kichwa na kuonyesha dole gumba kukubali.

(c) Muktadha usio rasmi wa shuleni wakati wa mapumziko/mazungumzo ya kawaida kati ya wanafunzi wawili (marafiki).

3. (a) Kikao cha daktari na mgonjwa, mwalimu na mwanafunzi darasani, kikao cha mahakama, au mahojiano ya kazi.

(b) Mazungumzo ya familia nyumbani, marafiki au watu wa rika moja wakipiga soga. Majibu zaidi yako katika sehemu ya **Kumbuka** katika ukurasa wa 7.

4. Shirikiana na mwenzako kufanya zoezi hili. Zingatieni vipengele vya usikilizaji husishi mlivyojifunza.

5. Unaweza kutumia kipakatalishi, simu, tabuleti au kompyuta kufanya zoezi hili. Tafiti tu kwenye mtandao salama ili ufanye mazoezi uliyopewa.

6. Fanya zoezi hili ukiwa na mwenzako. Hakikisha mnazingatia vipengele vya usikilizaji husishi mlivyojifunza.

ii. Kusikiliza kwa kutathmini
Jitathmini 1.6 (ukurasa wa 7-8)

1.
- Unazingatia uchambuzi wa hoja.
- Kupima ukweli wa mada inayozungumziwa.
- Kutathmini ufaafu wa mifano inayotolewa katika muktadha husika.

2. (a)
- Nuru na Asha wanachambua maana ya maadili ya kitaifa (uzalendo na uaminifu).
- Wanatathmini mifano halisi ya kuonyesha uzalendo shuleni kama vile kuheshimu bendera na kuzingatia usafi.
- Wanafanya maamuzi ya kufuata maadili hayo ili kuliletea taifa maendeleo.

(b) Muktadha usio rasmi shuleni ambapo wanafunzi wanatoka darasani wakitathmini somo walilofundishwa na mwalimu.

3. Rejelea majibu ya nambari ya 1 kufanya zoezi hili.

4. Unaweza kutumia kipakatalishi, simu, tabuleti au kompyuta kufanya zoezi hili. Tafiti tu kwenye mtandao salama ili ufanye mazoezi uliyopewa.

5. Fanya zoezi hili ukiwa na mzazi au mlezi wako. Hakikisha unatoa maoni yako kuhusu suala mnalolizungumzia.

2. Kusikiliza kwa kina

i. Sauti /dh/ na /th/
Jitathmini 2.1 (ukurasa wa 8-9)

1.(a) nidhamu, fedha

(b). theluthi, thelathini, thamani

2.

- Ili ujumbe ueleweke.

- Kuepuka kupotoka kwa ujumbe.

3.

- Hali ya kiakili ya mtu.
- Athari ya lugha ya kwanza.
- Maumbile ya mtu.
- Umri wa mtu.
- Kuwaza na kuzungumza kwa haraka.

4.(a) dha, dhe, dhi, dho, dhu.

(b). thi, thu, the, tha, tho.

5. (a). dhamani, adhiri, dhahabu, dhibiti, dhihaki, dhima, nidhamu, kudhihaki, idhinisha,udhuru,orodha, dharura, bidhaa, hifadhi,radhi, dhamana.

(b). Tamka maneno hayo kwa kuzingatia matamshi bora ya sauti /dh/.

(c). Tamka maneno yoyote kulingana na maelekezo. Kwa mfano: dhahabu, dhamana, dhawabu.

6. (a). theluji, thuluthi, thibitisha, thurea, thenashara, thabiti, thama, thawabu, thibitisho, thelathini, thumni, hadithi, athari, methali

(b). Tamka maneno hayo kwa kuzingatia matamshi bora ya sauti /th/.

(c). Tamka maneno yoyote kulingana na maelekezo. Kwa mfano: athari, thubutu, themanini.

7.(a) Soma sentensi ulizopewa kwa kuzingatia matamshi bora ya sauti /dh/ na /th/.

(b). (i) Dhahabu

(ii) dhidi

(iii) Mdhamini

(iv) Dhiki

(v) dhoruba

(c) (i) thamani

(ii) Hadithi

(iii) thelathini

(iv) thamani

(v) Athari

8. Unaweza kutumia kipakatalishi, simu, tabuleti au kompyuta kufanya zoezi hili. Tafiti tu kwenye mtandao salama ili ufanye mazoezi uliyopewa.

9. (a) Tamka jozi za maneno uliyopewa kwa kuzingatia matamshi bora ya sauti /dh/ na /th/.

(b) Tumia kamusi kutambua maana ya maneno uliyopewa kisha utunge sentensi sahihi.

10. (a)

- Nilidhani ningechelewa lakini nilifika salama katika thani chache zilizokuwa zimebaki.
- Mvuvi alipoteza thara yake ya kupimia samaki baada ya mawimbi makali kuleta madhara kubwa pwani.

(b) Tunga vitanzandimi sahihi vyenye sauti /dh/ na /th/.

(c) Zingatia matamshi bora ya sauti /dh/ na /th/.

ii. Sauti /g/ na /gh/
Jitathmini 2.2 (ukurasa wa 9-10)

1.(a). gari, gazeti, giza, gauni, gambusia, gane, gundi, gamu, gunia

(b). ghala, lugha, ghorofa, ghulamu, ghazi

2. (a). ga, gi, go, gu, ge

b. ghi, gha, ghu, ghe, gho

3. (a). **g**ari, **g**iza, **g**o**g**o, **g**umu, pi**g**a, te**g**a, **g**awa,ka**g**ua, mte**g**o, **g**oti, ta**g**a.

(b) Zingatia matamshi bora ya sauti /g/.

(c) Tamka maneno kama vile: mgonjwa, ufagio, gego

4 (a). **gh**ali, **gh**afla, **gh**orofa, **gh**uba, **gh**airi, lu**gh**a, ma**gh**aribi, shu**gh**uli, a**gh**alabu, mi**gh**ani.

(b) Tamka maneno uliyopewa ukizingatia matamshi bora ya sauti /gh/.

(c) ghadhibika, ghafla, ghali, ghalati, ghani

5 (a). Soma sentensi ulizopewa kwa kuzingatia matamshi bora ya sauti /g/ na /gh/.

(b) (i) gari

(ii) kukagua

(iii) gogo

(v) Upige

(c) (i) Ghali

(ii) magharibi, ghala

(iii) Ghafla

(iv) Lugha, shughuli

6. Unaweza kutumia kipakatalishi, simu, tabuleti au kompyuta kufanya zoezi hili. Tafiti tu kwenye mtandao salama ili ufanye mazoezi uliyopewa.

7. (a) Tamka maneno kwa usahihi ukizingatia matamshi bora ya sauti /g/ na /gh/.

   (b) Tumia kamusi kupata maana ya maneno kisha utunge sentensi sahihi.

8. (a)

- Gari lile lilikuwa la bei ghali.
- Mkulima alipokuwa akijenga ghala lake mtoto wake alienda kuwaburudisha wageni waliokuwa kwenye gala.
- Ghorofa ya kule kijijini ina golofa ambapo watoto huenda kucheza.

(b) Tumia kamusi kutafuta maana ya maneno mbalimbali yenye sauti /g/ na /gh/ kisha utunge vitanzandimi sahihi.

(c) Zingatia matamshi bora ya sauti /g/ na /gh/ unaposoma vitanzandimi.

iii. Sauti /b/ na /mb/

Jitathmini 2.3 (ukurasa wa 10-11)

1.(a). kitabu, kabati, bakuli, bakora, mabati, baba, kabuti

(b) mbaazi, nyumba, ng'ombe, mboga, mbata, mbuzi

2.(a). ba, bo, be, bi, bu

(b) mbi, mba, mbu, mbe, mbo

3.(a) baba, bata, bibi, boga, bubu, kaba, taba, beba, bati, boma, barabara, buni

(b).Tamka maneno uliyopewa kwa usahihi.

(c). Tamka maneno kama vile: bega, bata, bawabu

4. (a) mbuzi, mboga, mbele, mbivu, jambo, kwamba, chambua, nyumba, mbilikimo, ng'ombe, mbali

(b) Zingatia matamshi bora ya sauti /mb/.

(c) Tamka maneno kama vile: mbega, mbuni, mboni.

5. (b) i. baba

ii. bati

iii. Bado, dhoruba

iv. baraka, boma

v. bata

(c) i. mbuzi, mboga

ii. nyumba, mbali

iii. mbele

iv. jambo

v. mbawa

6. Unaweza kutumia kipakatalishi, simu, tabuleti au kompyuta kufanya zoezi hili. Tafiti tu kwenye mtandao salama ili ufanye mazoezi uliyopewa.

7. (a) Zingatia matamshi bora ya sauti /b/ na /mb/.

(b) Tumia kamusi kutafuta maana ya maneno uliyopewa yenye sauti /b/ na /mb/ kisha utunge sentensi sahihi.

(c) Zingatia matamshi bora ya sauti /b/ na /mb/ unaposoma vitanzandimi.

8. Hakikisha vitanzandimi unavyovitamka na kuvitunga vina sauti /b/ na /mb/ kisha ufanye ulivyoagizwa katika hayo mazoezi mengine.

9. Fanya zoezi hili na mzazi au mlezi wako. Hakikisha unazingatia matamshi bora ya sauti /b/ na /mb/.

iv. Sauti /d/ na /nd/

Jitathmini 2.4 (ukurasa wa 11-12)

1. (a) dada, dona, kidonda, udongo, daftari, darasa

(b) ndugu, kidonda, ndoa, kinanda, kitanda, kinda

2. (a) da, de, di, do, du

(b) nda, nde, ndi, ndo, ndu

3. (a) dinda, dunda, dondoa, udenda, dandalo, dundu

(b) dinda, dunda, dondoa, udenda, dandalo, dundu

4. Zingatia matamshi bora ya sauti /d/ na /nd/ katika maneno unayoyatamka.

5. (a) Soma sentensi kwa matamshi bora.

(b) Tamka maneno yafuatayo. (i) Dadangu (ii) akawasaidia (iii) Dengu (iv) Walidinda, kidijitali (v) madoa

(c) Tamka maneno yafuatayo. (i) rinda (ii) Alishinda (iii) kunde (iv) Walidinda (v) kitanda, kimetandikwa

6. Unaweza kutumia kipakatalishi, simu, tabuleti au kompyuta kufanya zoezi hili. Tafiti tu kwenye mtandao salama na utamke maneno unayoyapata.

7. Zingatia matamshi bora ya sauti /d/ na /nd/ katika jozi ulizopewa.

8. Hakikisha vitanzandimi unavyovitamka na kuvitunga vina sauti /d/ na /nd/ kisha ufanye ulivyoagizwa katika hayo mazoezi mengine.

9. Fanya zoezi hili ukiwa na mzazi au mlezi wako. Hakikisha umezingatia matamshi bora ya sauti /d/ na /nd/.

v. Sauti /k/ na /gh/

Jitathmini 2.5 (ukurasa wa 12)

1. (a) kaka, kitanda, kanganya, keti, kitabu, kiti

(b) ghere, bughudha, lugha, ghairi, ghali, gharama

2. (a) ka, ke, ki, ko, ku

(b) gha, ghe, ghi, gho, ghu

3. (a) kimbia, kamba, kombo, nakili, pokea, pikipiki

(b) gharama, bughudha, lugha, ghala, ughaibuni

4. Zingatia matamshi bora ya sauti /k/ na /gh/ katika maneno unayoyatamka.

5. (a) Soma sentensi kwa matamshi bora.

(b) Tamka maneno yafuatayo. (i) Duka (ii) kuweka (iii) ulizimika (iv) kucheza (v) marufuku

(c) Tamka maneno yafuatayo. (i) ghali (ii) Ghala (iii) ghafla (iv) Ghera (v) ghushi

6. Unaweza kutumia kipakatalishi, simu, tabuleti au kompyuta kufanya zoezi hili. Tafiti tu kwenye mtandao salama na utamke maneno unayoyapata.

7. Zingatia matamshi bora ya sauti /k/ na /gh/ katika jozi ulizopewa.

8. Hakikisha vitanzandimi unavyovitamka na kuvitunga vina sauti /k/ na /gh/ kisha ufanye ulivyoagizwa katika hayo mazoezi mengine.

9. Fanya zoezi hili ukiwa na mzazi au mlezi wako. Hakikisha umezingatia matamshi bora ya sauti /k/ na /gh/.

vi. Sauti /j/ na /nj/

Jitathmini 2.6 (ukurasa wa 12-13)

1. (a) jaa, kijani, kijiti, joto, kuja

(b) njaa, kunja, njama, onja

2. (a) ja, je, ji, jo, ju

(b) nja, nje, nji, njo, nju

3. (a) kuja, dijitali, kijiti, jaza, jitihada

(b) onja, kunja, punje, njiti, njoo, njiwa

4. Zingatia matamshi bora ya sauti /j/ na /nj/ katika maneno unayoyatamka.

5. Unaweza kutumia kipakatalishi, simu, tabuleti au kompyuta kufanya zoezi hili. Tafiti tu kwenye mtandao salama na utamke maneno unayoyapata.

6. Zingatia matamshi bora ya sauti /j/ na /nj/ katika jozi ulizopewa.

8. Hakikisha vitanzandimi unavyovitamka na kuvitunga vina sauti /j/ na /nj/ kisha ufanye ulivyoagizwa katika hayo mazoezi mengine.

9. Fanya zoezi hili ukiwa na mzazi au mlezi wako. Hakikisha umezingatia matamshi bora ya sauti /j/ na /nj/.

3. Matini ya kusikiliza

a. Kusikiliza kwa makini

Jitathmini 3.1 (ukurasa wa 13-14)

1. Ili kuelewa ujumbe unaopitishwa.

2 (a). Magonjwa ambukizi yanaweza kusambazwa kutoka kwa mtu mmoja hadi mwingine ilhali magonjwa yasiyoambukizwa hayawezi kupitishwa kutoka kwa mtu mmoja hadi mwingine. Mfano wa magonjwa ambukizi ni kama vile ugonjwa wa kifuakikuu. Magonjwa yasiyoambukizwa ni kama vile saratani, kiharusi, kisukari na ugonjwa wa moyo. Mbinu za kuepuka magonjwa ambukizi ni kama vile kuvaa maski na kupimwa mtu anapokisia kuwa ni

mgonjwa. Kufanya mazoezi na kula vyakula kwa uangalifu kunazuia magonjwa yasiyoambukizwa.

(c). (i) Ugua- shikwa au patwa na maradhi.

(ii) Sambaza - eneza kitu kama vile ugonjwa.

(iii) Ndwele - ugonjwa

(iv). Salia - bakia

(v). Barakoa - aina ya kitambaa chembamba kinachofunika pua na mdomo ili kuzuia viini.

3. Unaweza kutumia kipakatalishi, simu, tabuleti au kompyuta kufanya zoezi hili.

(b) Kusikiliza kwa kufasiri

Jitathmini 3.2 (ukurasa wa 14-15)

1. Kusikiliza kifungu kinachosomwa kwa lengo la kuuelewa ujumbe kwa undani.

2.

- Kuzingatia kiimbo na toni ya mwasilishaji.
- Kuelewa muktadha au mazingira ya kifungu.
- Kusoma ishara za mwili za mwasilishaji.

3. (a). Usalama shuleni

(b).

- Usalama wa mazingira na majengo - majengo imara yenye hewa safi, nyaya za stima zilizokingwa na viwanja salama vya michezo.
- Usalama wa kisaikolojia - kupiga marufuku uonevu, dhihaka na matusi ili wanafunzi waheshimiane.
- Maandalizi na mafunzo ya dharura - kuwafunza wanafunzi jinsi ya kukabili majanga, kutumia vifaa vya kuzima moto na kujiokoa.

(c).

- Chupa zilizovunjika.
- Mashimo yaliyo wazi.
- Nyaya za stima zisizokingwa.

(d). Kuwafunza wanafunzi jinsi ya kutumia vifaa vya kuzima moto, jinsi ya kutoka majengoni kwa utaratibu dharura inapotokea na kufanya mazoezi ya mara kwa mara ya kukabiliana na majanga ili kuwajengea ujasiri na maarifa ya kujiokoa.

(e).

(i) Mazingira - eneo linalomzunguka mwanafunzi; anakojifunzia au kuchezea.

(ii) Dharura - Hali ya hatari ya ghafla au janga lisilotazamiwa na linalohitaji hatua za haraka kuchukuliwa.

4.

- Vifaa vya zima moto kuwa kila mahali.
- Mazingira safi.
- Wanafunzi kuwa na ujuzi kuhusu jinsi ya kushughulikia dharura yoyote.
- Nyaya za stima zimekingwa.
- Majengo yana milango ya dharura.
- Hakuna chupa zilizovunjika.

5. (a). Unaweza kutumia kipakatalishi, simu, tabuleti au kompyuta kufanya zoezi hili.

(b).

- Kusikiliza kwa makini
- Kuzingatia toni na kiimbo katika video.
- Kuangalia ishara za uso.

6. Fanya zoezi hili ukiwa na mzazi au mlezi wako.

(c) Kusikiliza kwa ufahamu

Jitathmini 3.3 (ukurasa wa 15-16)

1. Kupokea taarifa na kuelewa ujumbe unaopitishwa.

2. (b) Mwanamke na mwanamume kusaidiana kutekeleza majukumu ya nyumbani.

(c) Dime, Mjomba

(d) ndoa, mapenzi, uwajibikaji, umoja na ushirikiano, ubabedume/ taasubi ya kiume, kazi

(e) ...ametulia kama maji mtungini

(f) (i) tetesi/ nong'ono (ii) nimwachie majukumu mengi (iii) hali ya kumthamini mwanamume zaidi ya mwanamke

3. Hakiki hoja unazozitoa kwa kuzingatia sehemu ya **Kumbuka** katika ukurasa wa 15-16.

4. Hakiki hoja unazozitoa kwa kuzingatia sehemu ya **Kumbuka** katika ukurasa wa 16.

5. Hakiki kanuni unazozitaja kwa kuzingatia sehemu ya **Kumbuka** katika ukurasa wa 15-16. Pia, jibu maswali hayo mengine kulingana na ufahamu uliousikiliza kutoka kwa mgeni mwalikwa.

6. Unaweza kutumia kipakatalishi, simu, tabuleti au kompyuta kufanya zoezi hili. Tafiti tu kwenye mtandao salama na ufanye mazoezi uliyopewa.

4. Kuzungumza

a. Kuzungumza ili kupasha habari

Jitathmini 4.1 (ukurasa wa 16-17)

1. Mkutanoni kiongozi anapowasilisha habari muhimu, darasani mwalimu au mgeni mwalikwa anapofundisha kuhusu mada fulani, hospitalini daktari akimweleza mgonjwa masharti ya kuzingatia, redioni au runingani mtangazaji akitoa habari kuhusu jambo fulani.

3.

- Kutafiti kuhusu mada ili kupeana ujumbe ulio sahihi.
- Kuandika hoja atakazowasilisha kwa wanafunzi.
- Kujua hadhira yake.

4.

- Kutumia lugha inayofaa ili kuhakikisha kuwa hadhira inaelewa kwa wepesi.
- Kutambua hadhira inayozungumziwa ili kuhakikisha mada na lugha zinalingana na hadhira hiyo.
- Kutumia ishara wakati wa mazungumzo kama vile kuitazama hadhira ana kwa ana.
- Kutoa mifano husika wakati wa mazungumzo ili wanaozungumziwa waelewe kwa urahisi.

5. Wanafunzi wanapashwa habari kuhusu ulangunzi wa binadamu na jinsi ya kujikinga dhidi ya walanguzi.

6. Hakiki vipengele unavyovitoa kwa kurejelea sehemu ya **Kumbuka** katika ukurasa wa 17.

7.

- Mazungumzo ya kuelekeza kuhusu jinsi ya kutumia kitu fulani.
- Mazungumzo ya kuelimisha kuhusu mada fulani.
- Mazungumzo ya kutoa tahadhari kuhusu hatari fulani.
- Mazungumzo ya kutangaza kuhusu jambo fulani.

8. Unaweza kutumia kipakatalishi, simu, tabuleti au kompyuta kufanya zoezi hili. Tafiti tu kwenye mtandao salama na ufanye mazoezi uliyopewa.

9. Zingatia maagizo uliyopewa katika kufanya zoezi hili.

b. Uzungumzaji wa papo kwa hapo

Jitathmini 4.2 (ukurasa wa 17-18)

1. Tathmini hoja zako kwa kurejelea sehemu ya **Kumbuka** katika ukurasa wa 18.

3. Uzungumzaji wa papo kwa hapo ni uzungumzaji wa ghafla, unaohusisha watu kuzungumza bila matayarisho yoyote.

4.

- Hali shuleni
- Uhalifu mitandaoni
- Kutia bidii shuleni.

5.

- Ubunifu - Mzungumzaji anapaswa kuwa mbunifu kwani mazungumzo haya ni ya ghafla na hayatoi muda wa kujitayarisha.
- Ukakamavu - Mzungumzaji anapaswa kuzungumza bila woga.
- Lugha ya kawaida - Haya ni mazungumzo ya kawaida, hivyo lugha ya kawaida inapaswa kutumika ili kueleweka kwa urahisi.
- Matumizi ya ishara - Ni muhimu kuitazama hadhira moja kwa moja unapoizungumzia.
- Matumizi ya kiwango kifaacho cha sauti - Ni vyema kutumia sauti itakayosikika vizuri. Sauti iwe ya kiwango cha wastani; si ya juu sana na si ya chini sana.

c. Uzungumzaji wa kushawishi

Jitathmini 4.3 (ukurasa wa 18-19)

1.

- Tafiti kuhusu suala utakalolizungumzia.
- Tumia lugha inayoafiki kiwango cha wasikilizaji.
- Tumia mifano mwafaka kufafanua hoja zako.

3. Haya ni mazungumzo ya kushawishi

4.

- Hutumia lugha inayovuta hisia za wasikilizaji.
- Mzungumzaji hutumia sauti yenye mvuto kwa hadhira.
- Matumizi ya mkazo wa maneno yenye uzito ili kuishawishi hadhira.
- Kuzungumza kwa ufasaha ili hadhira iweze kupata ujumbe sahihi.
- Ukakamavu na kujiamini kwa mzungumzaji ili kuonyesha kuwa ana imani na kile anachokizungumzia
- Kurudiwarudiwa kwa hoja muhimu ili ziweze kukumbukwa na hadhira

5. Unaweza kutumia kipakatalishi, simu, tabuleti au kompyuta kufanya zoezi hili.

6. Fuata maagizo uliyopewa kufanya zoezi hili.

d. Kuzungumza kwa kuambatanisha na vitendo au ishara
Jitathmini 4.4 (ukurasa wa 19-21)

1.

- kuinua mikono
- kutikisa kichwa (kukubali au kukataa)
- kuelekeza kidole
- kutabasamu

- kupiga makofi
- kuiga vitendo halisi (kama kufagia au kuonyesha saa).

2.(a) Majukumu na wajibu wa watoto nyumbani na shuleni (kama kusoma kwa bidii, kuzingatia usafi, na heshima).

(b) Ni aina ya mawasiliano ambapo maneno yanayosemwa yanaungwa mkono na miondoko ya mwili, ishara za mikono au sura ya uso ili kufafanua na kusititiza ujumbe.

(c)

- huvutia usikivu
- hutambulisha hisia za mzungumzaji,
- husaidia ujumbe kueleweka na kukumbukwa kwa urahisi
- huleta ladha au mvuto katika mazungumzo.

(d)

- Mwalimu aliwaonyesha waketi kwa ishara ya mkono,
- Baraka aliigiza kufagia kwa mikono
- Furaha aliweka kitambaa puani kuonyesha harufu mbaya
- Amani alipeana mkono na Neema kuonyesha urafiki.

3. Zingatia ishara na vitendo vifaavyo.
4. Fanya zoezi hili katika mtandao salama.
5. Hakiki hoja zako kwa kurejelea sehemu ya **Kumbuka** katika ukurasa wa 20.
6. Unaweza kutumia kipakatalishi, simu, tabuleti au kompyuta kufanya zoezi hili.
7. Zingatia ishara na vitendo vifaavyo.
8. Fanya zoezi hili na mzazi au mlezi wako. Zingatia vitendo na ishara zinazofaa.

e. Kuzungumza kwa kutumia vidokezo vya hoja
Jitathmini 4.5 (ukurasa wa 21-22)

1.

- Ili kutosahau hoja muhimu
- Kuwa na mtiririko mzuri wa mawazo
- Kutumia muda vizuri
- Kuongeza kujiamini/ ukakamavu mbele ya watu.

2. (a)

- Haki ya kupata elimu bora.
- Haki ya kupata chakula bora na malazi/makazi safi.
- Haki ya kupata huduma za afya na chanjo.
- Haki ya kulindwa dhidi ya ukatili, unyanyasaji na ubaguzi.
- Haki ya kutoa maoni na kusikilizwa.
- Haki ya kucheza na kupumzika.

(b) Mazungumzo haya yanatokea katika muktadha wa shuleni (darasani) wakati wa kazi ya vikundi ya somo la Kiswahili.

(c)

- Inawasaidia wanafunzi kujadili mada kwa utaratibu bila kurudia hoja au kupoteza mada kuu
- huokoa muda
- huongeza kujiamini
- huboresha mawasiliano
- huongeza mpangilio wa mawazo.

(d)

- Walibainisha kiini cha mada (haki za watoto).

- Walipanga mawazo kimantiki (hoja ya kwanza hadi ya mwisho).
- Waliandika vidokezo kwenye daftari ili kuvirejelea.

5. Unaweza kutumia kipakatalishi, simu, tabuleti au kompyuta kufanya zoezi hili. Hakiki umuhimu wa kutumia vidokezo unaoutaja kwa kurejelea sehemu ya **Kumbuka** katika ukurasa wa 22.
6. Fanya zoezi hili na mzazi au mlezi wako.

f. Uzungumzaji katika sherehe
Jitathmini 4.6 (ukurasa wa 22-23)

1.
- Kutambua aina ya sherehe na muktadha wake (rasmi au isiyo rasmi).
- Kutumia lugha inayoifaa hadhira iliyohudhuria.
- Kujikita kwenye kiini cha sherehe.
- Kutumia ishara, sauti na hisia zinazoendana na ujumbe (furaha au huzuni).

2. (a) Ni mawasiliano au hotuba zinazotolewa wakati wa hafla, shughuli au maadhimisho maalumu ili kutoa taarifa, burudani au kueleza hisia.
(b) Sherehe rasmi ya shule ya kuhamasisha haki za kibinadamu mbele ya wageni waheshimiwa, walimu na wanafunzi.
(c) Haki za kibinadamu ni za kila mtu bila ubaguzi; jamii inapaswa kulinda wanyonge (watoto, wanawake, wenye mahitaji maalum) ili kujenga amani na maendeleo.
(d)
- Wazungumzaji walitumia lugha rasmi ya heshima ("Wageni waheshimiwa...").
- Walikuwa na tabasamu na ishara za msisitizo (kuinua mkono, kupiga makofi).
- Walizingatia kiini cha sherehe hadi mwisho, maamkuzi yafaayo na kutoa ujumbe mkuu.

3. Unaweza kutumia kipakatalishi, simu, tabuleti au kompyuta kufanya mazoezi haya.
4. Zingatia vipengele vya uzungumzaji katika sherehe.

5. Mazungumzo mahususi

(a) Maamkuzi na maagano

Jitathmini 5.1 (ukurasa wa 24-25)

1. (a) Hakiki majibu yako kwa kurejelea sehemu ya **Kumbuka** katika ukurasa wa 25.

(b) Hakiki majibu yako kwa kurejelea sehemu ya **Kumbuka** katika ukurasa wa 25.

(c) Habari za asubuhi? – Njema, Sabalheri! – Aheri, Hujambo! – Sijambo, Shikamoo! – Marahaba, Salaam aleikum! – Aleikum salaam!, Umeshindaje? – Vyema

2. (a) Hakiki majibu yako kwa kurejelea sehemu ya **Kumbuka** katika ukurasa wa 25.

(b) Lala salama! – Lala salama pia!, Kwaheri! – Kwaheri ya kuonana!, Jioni njema! – Nawe pia!, Alamsiki! – Binuru!, Tutaonana! – Majaaliwa!, Safari njema! – Asante!

3. (a) Soma mazungumzo kwa kuzingatia matamshi bora.

(b) Hujambo – Sijambo, Shikamoo! – Marahaba!

(c) Shikamoo! – Marahaba!

(d) Kwaheri. – Kwaheri ya kuonana.

4. Unaweza kutumia kipakatalishi, simu, tabuleti au kompyuta kufanya zoezi hili. Tafiti tu kwenye mtandao salama kisha ufanye mazoezi uliyopewa.

5. Mnapoigiza, hakikisha umezingatia maamkuzi na maagano mwafaka uliyojifunza.

6. Fanya zoezi hili ukiwa na mzazi au mlezi wako. Hakikisha umezingatia maamkuzi na maagano mwafaka uliyojifunza.

b. Kusikiliza maagizo

Jitathmini 5.2 (ukurasa wa 25-26)

1. (a), (b), (d)

2. (a) kamilisha kazi hiyo mapema, makinika unapofanya kazi

(b) Jibu maswali yote, hakikisha kurasa zote zimepigwa chapa

(c) fungua madirisha, andika daftarini

(d) fuata sheria za shule, kila mtu anafaa kuvaa sare ya shule

3. Katika tathmini – Jubu maswali yote

- Kutoa wito – Njoo hapa.
- Kazini – Shirikiana kufanya kazi hiyo.
- Shuleni – Madarasa yote yawekwe kamera za siri.
- Nyumbani – Osha vyombo vilivyotumika.

4. (a) Soma mazungumzo hayo kwa kuzingatia matamshi bora.

(b)

- Vaa glavu hizi.
- Nenda utuchotee maji.
- Utaifinya kidogo halafu uizungushe upande wa kushoto.
- Weka sabuni ya unga kwenye maji kabla ya kupiga deki.
- Ngoja sakafu ikauke kwanza kabla uikanyage.

5. Hakiki majibu yako kwa kurejelea sehemu ya **Kumbuka** katika ukurasa wa 26.

6. Hakiki majibu yako kwa kurejelea sehemu ya **Kumbuka** katika ukurasa wa 26.

7. Unaweza kutumia kipakatalishi, simu, tabuleti au kompyuta kufanya zoezi hili. Tafiti tu kwenye mtandao salama kisha ufanye mazoezi uliyopewa.

8. Mnapoigiza, hakikisha umezingatia sifa za kimsingi za maagizo ulizojifunza.

9. Fanya zoezi hili ukiwa na mzazi au mlezi wako. Hakikisha umezingatia maamkuzi na maagano mwafaka uliyojifunza.

6. Tanzu za fasihi

Fasihi simulizi

Jitathmini 6.1 (ukurasa wa 27)

1. Fasihi inahusika na kuwasilisha ujumbe, kuelimisha, kuadilisha, kutoa burudani na kuhifadhi utamaduni pamoja na historia ya jamii kwa kutumia lugha na ishara za kisanaa.
2. (a)
   - Huwasilishwa kwa njia ya mdomo.
   - Huwa na fanani/msimulizi anayeonana ana kwa ana na hadhira yake.
   - Huambatana na utendaji (vitendo na ishara).
   - Ni mali ya jamii nzima na huhifadhiwa akilini.
   - Huwa na fomyula ya kuanzia na kumalizia.

   (b)

Nyimbo na ushairi, Hadithi/ Ngano, Semi, Mazungumzo na Maigizo.

Fasihi andishi
Jitathmini 6.2 (ukurasa wa 27)

1.
   - Huhifadhiwa katika maandishi na huwasilishwa kwa njia ya maandishi.
   - Huwa na fanani/msimulizi asiyeonana ana kwa ana na hadhira.
   - Ni mali ya mtu binafsi (mwandishi).
   - Husomwa mahali popote na wakati wowote.
   - Haiwezi kubadilika, kushauliwa, wala kuvurugika kwa urahisi kwa vile imeandikwa.

2. Hadithi fupi, Riwaya, Tamthilia, Novela na Ushairi.
3.

Fasihi simulizi	**Fasihi andishi**
Huwasilishwa kwa njia ya mdomo	Huwasilishwa kwa njia ya maaandishi
Ni mali ya jamii	Ni mali ya mtu binafsi
Hadhira yake ni hai/tendi	Hadhira yake ni tuli
Huambatana na utendaji	Haiambatani na utendaji
Inaweza kubadilika	Haiwezi kubadilika
Huwasilishwa mahali maalum	Husomwa mahali popote
Huwasilishwa wakati maalum hasa jioni	Husomwa wakati wowote

Ina tanzu na vipera vingi	Tanzu na vipera vyake ni vichache
Huhifadhiwa akili	Huhifadhiwa vitabuni
Ni kongwe kuliko andishi	Ni ya hivi majuzi baada ya uvumbuzi wa maandishi

4.
- Kutumia fomula ya kufungua na kufunga.
- Kuishirikisha hadhira kupitia kwa maswali na nyimbo.

5. Unaweza kutumia kipakatalishi, simu, tabuleti au kompyuta kufanya zoezi hili.
6. Fanya zoezi hili na mzazi au mlezi wako.

a. Hadithi

i. Mighani

Jitathmini 6.3 (ukurasa wa 27-29)

1.
- Kutumia lugha kulingana na kiwango cha hadhira.
- Kuwa na ujasiri mbele ya hadhira.
- Kubadilisha kiimbo (kupanda na kushuka kwa sauti) kulingana na matukio.
- Kuigiza baadhi ya matukio (mfano: jinsi shujaa alivyopigana au kutembea).
- Kutumia ishara za uso na mikono, na kuvaa maleba (mavazi) maalumu yanayoafikiana na hadithi.

2. (a)
- Njue alikuwa na nguvu, hekima, na ujasiri mkubwa wa kukabiliana na simba mkali na wavamizi.
- Kutetea wanyonge: Njue alijitolea kuokoa jamii yake dhidi ya njaa na maadui.
- Kifo kutokana na usaliti/chuki: Njue aliuawa vitani baada ya baadhi ya watu kumwonea wivu na kupanga njama dhidi yake.
- Kuhifadhiwa kwa kumbukumbu: Wazee waliamua hadithi yake isimuliwe kizazi baada ya kizazi ili kuwafunza vijana.
- Huaminika kuwa na ukweli fulani wa kihistoria.
- Hutumia chuku kusifia matendo ya shujaa.

(b) Inadhihirisha matumizi ya kiimbo na hisia (huzuni wakati wa kifo chake, ujasiri wakati wa kupigana na simba), na utendaji kupitia maelezo ya jinsi Njue alivyobeba fimbo na mkuki.

(c)
- Umoja ni nguvu (wananchi walipoungana walishinda ukame).
- Umuhimu wa ujasiri, uzalendo na kujitolea kwa ajili ya maslahi ya jamii.
- Madhara ya wivu na chuki katika jamii.

(d)
- Lugha iliyotumika ni ya kisanaa na sahali inayotiririka vizuri. Inatumia fomula ya kuanzia ya hadithi simulizi ("Hapo zamani za kale...") na ina sifa za chuku na ushawishi wa kimaadili.

4. Unaweza kutumia kipakatalishi, simu, tabuleti au kompyuta kufanya zoezi hili.
5. Zingatia vipengele vifaavyo vya kuwasilisha mighani.

ii. Hurafa

Jitathmini 6.4 (ukurasa wa 29-30)

4 (a). Hurafa ni hadithi ambazo wahusika ni wanyama ambao wamepewa tabia na sifa za binadamu. Katika hadithi hii Sungura na Fisi wamepewa uwezo wa kuzungumza.

(b). Ni muhimu kushirikiana na wenzako katika kufanya kazi.

5.

- Hadhira: ili ujumbe na lugha iwe ni ya kiwango cha hadhira
- Mazingira: ili utoe mifano ukitumia vifaa vinavyopatikana kwenye mazingira hayo.
- Lugha ya hadhira: ni lazima utumie lugha ambayo hadhira wanielewa.
- Maleba: mavazi yanatsahili kuoana na kile kinachowasilishwa.
- Ishara za mwili zinapaswa kuoana na ujumbe ulio kwenye hadithi.

7. Unaweza kutumia kipakatalishi, simu, tabuleti au kompyuta kufanya zoezi hili.
8. Fanya zoezi hili na mzazi au mlezi wako.

iii. Hekaya

Jitathmini 6.5 (ukurasa wa 30)

1(a). Ni hadithi ambayo mhusika mmoja hutumia ulaghai ili kujinufaisha kutoka kwa mhusika mwingine.

(b). Watu wanaotumia ujanja ili kufaidika huwa na mwisho mbaya.

2.

- Hadhira - ili nitumie lugha ya kiwango chao.
- Kuvalia maleba maalumu.
- Kuigiza matendo kulingana na ujumbe wa hadithi.
- Kubadilisha toni kulingana na hadithi.

3. Zingatia vipengele vya kuwasilisha hekaya.

4. Unaweza kutumia kipakatalishi, simu, tabuleti au kompyuta kufanya zoezi hili.

5. Hekaya ni hadithi ambayo mhusika hutumia ujanja ili kufaidika kutoka kwa mhusika mwingine ilhali hurafa ni hadithi ambazo wahusika ni wanyama ambao hupewa sifa na tabia za binadamu.

6. Fanya zoezi hili na mzazi au mlezi wako.

Matumizi ya lugha katika hadithi

Jitathmini 6.6 (ukurasa 30-31)

1. Methali, tashbihi, nahau, takriri
2.
    - Huipa hadithi mvuto
    - Huwasilisha ujumbe mzito kwa lugha ya mkato
    - Hupunguza ukinaifu wa kutumia lugha ya kawaida
    - Huimarisha ubunifu

3. (a) Methali, nahau
   (b) Methali imetumika kutoa funzo kwa msomaji na mhusika Baraka; Nahau imetumika kuipamba hadithi na kuiongezea mvuto.
   (c) Mzembe hafi maskini – Mtu mvivu huishi maisha ya umaskini ikiwa hawezi kujitahidi kufanya kazi ili kujikimu.

4. Fanya zoezi hili katika mtandao salama.

5. Shirikiana na wenzako kufanya zoezi hili. Zingatia mambo yaliyoorodheshwa katika zoezi hili.

6. Tumia vipengele vya lugha kama ujumbe, methali, tashbihi, nahau na urudiaji wa maneno unapofanya zoezi hili.

7. Zingatia matumizi ya vipengele vya lugha katika hadithi yako.

8. Wawasilishie wenzako hadithi uliyoitunga.

9. Unaweza kutumia kipakatalishi, simu, tabuleti au kompyuta kufanya zoezi hili.

10. Fanya zoezi hili na mzazi au mlezi wako.

Wahusika katika hadithi

Jitathmini 6.7 (ukurasa wa 31-32)

1. Wahusika hao wanaweza kuwa watu, wanyama, miungu, miti, milima, miamba au majitu.

2. Isome au msomeane hadithi hiyo kwa zamu.

3. (a) Babu, Wajukuu

(b) Swara, Kiboko, Tausi, Chiriku, Kifaru, Simba, Kobe, Duma

(c) Swara – amewajibika kwa vile uongozi wake haukuwa na tatizo

Kiboko - amewajibika kwa vile uongozi wake haukuwa na tatizo

Tausi – dikteta/ mbaguzi kwa vile aliamua kuwa wale waliohudhuria sherehe hiyo wangefuata tu mila za ukoo wake. Pia, ni mwenye majivuno.

Chiriku – mtetezi wa haki kwa vile alijaribu kujitetea kuwa hakuwa na uwezo wa kuchanua mkia kama Tausi

Kifaru na Simba – wametamauka kwa vile waliketi kando kwa vile walijua kuwa hawangeweza kuchanua mkia wala kucheza kwa madaha.

Kobe – mwenye busara kwa vile alimshauri Tausi kuwa kila mnyama alikuwa na utamaduni tofauti uliofaa kuheshimiwa.

(d) Kila mnyama ana utamaduni wake ambao unafaa kuheshimiwa na wanyama wengine, kila mnyama ana uwezo tofauti na wanyama hawafai kubagua wanyama wengine.

4. Unaweza kutumia kipakatalishi, simu, tabuleti au kompyuta kufanya zoezi hili. Tafiti tu kwenye mtandao salama kisha ufanye mazoezi uliyopewa.

5. Unapotunga hadithi fupi na kuwatambia wenzako, hakikisha ina wahusika wanyama.

6. Fanya zoezi hili ukiwa na mzazi au mlezi wako. Hakikisha unazingatia mojawapo ya hadithi uliyoisikiliza.

b. Semi

Tashbihi, sitiari na methali

Jitathmini 6.8 (ukurasa wa 32-34)

1.
- Tunatumia tamathali za usemi kama vile tashbihi (kufananisha kwa kutumia viunganishi)
- Sitiari (kufananisha moja kwa moja)
- Methali (semi fupi zenye hekima na maana ya ndani).

2. (a)
- "...wewe ni mwangaza *kama* taa gizani..."
- "...mioyo yetu ni myepesi *kama* manyoya ya ndege..."

(b)
- Kujenga picha/taswira akilini mwa msikilizaji.
- Kufafanua jambo kwa ulinganifu.
- Kuongeza mvuto wa lugha ili kuzuia uchovu (ukinaifu).

3 (b) "Tembo ni nguzo ya hekima..."
(c)
- Kujenga picha/taswira akilini mwa msikilizaji.
- Kufafanua jambo kwa ulinganifu.
- Kuongeza mvuto wa lugha ili kuzuia uchovu (ukinaifu).

4 (a).
- "Asiyefunzwa na mamaye hufunzwa na ulimwengu."
- "Umoja ni nguvu, utengano ni udhaifu."

(b)
- Zina maana ya juu (wazi) na maana ya ndani (fumbo/ujumbe).
- Zimebeba hekima na maarifa ya kiasili ya jamii.
- Zina mdundo wa kishairi na maneno machache yenye uzito mkubwa.

(c)
- Kuelimisha.
- Kuonya dhidi ya tabia mbaya.
- Kutoa ushauri na mwongozo wa maisha.
- Kufanya lugha iwe ya kuvutia.

5. Unaweza kutumia kipakatalishi, simu, tabuleti au kompyuta kufanya zoezi hili.
6. Fanya zoezi hili ukishirikiana na mwenzako.
7. Fanya zoezi hili na mzazi au mlezi wako.

iv. Vitendawili

Jitathmini 6.9 (ukurasa wa 34-35)

1.

- Matumizi ya kiwango cha sauti kifaacho ili hadhira iweze kusikia.
- Kuzingatia mila na tamaduni za jamii husika ili iweze kuelewa na kukitegua kitendawili.
- Kushirikisha hadhira kujibu vitendawili ili shughuli za utegaji na uteguaji wa vitendawili zifaulu.
- Kutumia ishara zifaazo kama vile kutazama hadhira ana kwa ana.
- Kutamka maneno inavyofaa ili hadhira ipate ujumbe uliokusudiwa.
- Kuzingatia umri wa hadhira ili mtegaji aweze kuteua vitendawili vinavyolingana na umri wao.

3. Hakiki majibu yako kwa kurejelea sehemu ya **Kumbuka** katika ukurasa wa 34.

4.
(a) Yai
(b) Giza
(c) Kivuli
(d) Muwa
(e) Kisogo

5. Fanya zoezi hili na mzazi au mlezi wako.
6. Unaweza kutumia kipakatalishi, simu, tabuleti au kompyuta kufanya zoezi hili.
7. Fanya zoezi hili na mzazi au mlezi wako.

e. Nahau
Jitathmini 6.10 (ukurasa wa 35-36)

1.

- Ili kuboresha lugha zinapotumika katika maandishi au mazungumzo.
- Ili kupunguza ukali wa lugha hasa mtu anapotaka kutumia tasfida.
- Ili kukuza msamiati wa lugha.
- Ili kuweza kuficha siri kwa kuwa maneno yanayotumika yana maana fiche.

3.(a)

- Panga njama
- Simama kidete
- Pigwa na butwaa
- Piga moyo konde
- Fua dafu
- Kunja uso

(b).

- Panga njama - panga kufanya jambo ambalo limefichwa au la siri
- Simama kidete - kuwa na msimamo dhabiti
- Pigwa na butwaa - shtuka

- Piga moyo konde - fanya uamuzi mgumu
- Fua dafu - faulu
- Kunja uso - kasirika

4.

(a) Shtaki njaa - kula

(b) Kula kalenda – fungwa jela

(c) Piga chafya – toa hewa puani bila kutarajia

(d) Piga deki – safisha sakafu kwa kutumia maji na kitambaa au matamvua

(e) Enda mrama - haribika kwa jambo

(f) Asi ukapera - oa

5. (a). piga mbizi

(b). shika hatamu

(c). pata nafuu

(d). piga kura

(e). piga deki

6. Tunga sentensi zinazodhihirisha matumizi sahihi ya nahau ulizopewa. Kwa mfano:

(a) Alipopata mafua alipiga chafya.

(b) Baada ya muda mrefu Juma aliasi ukapera.

(c) Baada ya kupata jiko, Yona alibadilika.

(d) Shule yetu imepiga hatua katika mchezo wa kandanda.

(e) Mzee Mambo alikunja uso baada ya kushindwa katika uchaguzi.

7. Unaweza kutumia kipakatalishi, simu, tabuleti au kompyuta kufanya zoezi hili.

c. Nyimbo

i. Nyimbo za watoto
Jitathmini 6.11 (ukurasa wa 36-37)

2 (a). Nyimbo za watoto huimbwa na watoto wakati wanapocheza.

(b).

- Huimbwa kwa kurudiarudia maneno ili kusisitiza ujumbe.
- Huwa na sentensi au kauli fupifupi kwa vile zinaimbwa na watoto, ili waweze kukumbuka kwa haraka.
- Huimbwa na watoto katika michezo yao ya kitoto.

- Huandamana na miondoko ya mwili na muziki.
- Hutungwa kwa ajili ya watoto.
- Huweza kutungwa na watoto wenyewe au mtu mwingine.
- Huweza kuimbwa na watoto wenyewe au watu wengine huku watoto wakisikiliza.
- Huhusu mambo yanayowaathiri na kuwavutia watoto.
- Hutumia lugha nyepesi inayoeleweka na watoto.

(c).

- Miondoko ya mwili kama vile kunengua viuno, kuzungukazunguka na kupiga makofi.
- Kurudiarudia maneno ili kusisitiza ujumbe wa wimbo.
- Huwasilishwa na watoto wenyewe hasa wakati wao wa michezo.
- Mara nyingi, nyimbo hizo huandamana na uigizaji kama vile kuruka, kukimbia na hata kucheka.
- Huandamana na matumizi ya maneno yasiyo na maana kamili ila ya mchezo tu.
- Huweza kuimbwa taratibu au kwa kasi kwa kutegemea aina ya mchezo unaoandamana na wimbo husika.
- Mtoto mmoja anaweza kuimba ubeti mzima huku wenzake wakishirikiana naye kuimba kibwagizo.

3. Hakiki majibu yako kwa kurejelea sehemu ya **Kumbuka** katika ukurasa wa 36-37.

4. Unaweza kutumia kipakatalishi, simu, tabuleti au kompyuta kufanya zoezi hili.

7. Fanya zoezi hili na mzazi au mlezi wako.

ii. Bembelezi
Jitathmini 6.12 (ukurasa wa 37-38)

1.

- Kutumia sauti ya chini na laini ili kumliwaza au kumtuliza mtoto.
- Urudiaji wa maneno ili kusisitiza ujumbe.
- Kuchezesha viungo vya mwili hasa mtu anapombembeleza mtoto.
- Kutumia lugha ya kushawishi ili kumshawishi mtoto alale.
- Mwasilishaji hupandisha na kushusha sauti kulingana na hisia anazotaka kuwasilisha.
- Kuandamana na uigizaji, kwa mfano ikiwa mtoto analia, uigizaji utamfanya mtoto kunyamaza na hata kufurahia.
- Kuzungumza moja kwa moja na yule anayeimbiwa.

2. (b) Wimbo wa bembelezi huimbwa na mlezi kwa mtoto, ili mtoto aache kulia au alale.

(c).

- Huimbwa kwa sauti ya chini ili kumliwaza mtoto au kumfanya alale.
- Huwa na urudiaji wa maneno ili kusisitiza ujumbe.

- Hutumia lugha shawishi ili kumfanya mtoto anyamaze au alale.
- Huimbwa na wazazi au walezi wa watoto wanaoimbiwa.
- Mara nyingi, hutoa ahadi na zawadi kwa mtoto, hasa akiwa mtiifu.
- Humsifu mtoto na kumwambia maneno matamu au ya kupendeza ili akubali kufanya anachoambiwa.
- Hutumia maneno mepesi ili mtoto ayaelewe kwa urahisi.
- Mara nyingi huandamana na kusukwasukwa kwa mtoto ili kumbembeleza alale au aache kulia

(d). Wimbo huu huwasilishwa kwa sauti ya chini na kurudiarudia maneno.

4. Unaweza kutumia kipakatalishi, simu, tabuleti au kompyuta kufanya zoezi hili.

7. Fanya zoezi hili na mzazi au mlezi wako.

iii. Nyimbo za kazi
Jitathmini 6.13 (ukurasa wa 38)

1. Nyimbo kazi huimbwa na mtu yeyote wakati anapofanya kazi.

2. Huweza kuimbwa shambani, baharini au katika mandhari ambamo kazi inafanyika.

4.

- Umeimbwa na kikundi cha watu: wakulima.
- Matumizi ya lugha inayoeleweka kwa urahisi kama vile jasho la leo ndio siri ya mavuno.
- Wimbo huu umetumia urudiaji
- Wimbo huu unaambatana na shughuli ya kilimo.

5.

- Kuhamasisha watu kutia bidii.
- Huhimiza utangamano miongoni mwa wafanyakazi.
- Hutumiwa kama kitulizo kwa wanaofanya kazi.
- Hutumiwa kukashifu uvivu.

6.

- Wimbo huu unawahimiza watu kuchangamkia shughuli za shambani ili kuepuka njaa.
- Unatoa wito kwa watu watie bidii katika kazi yao ya ukulima ili waepuke njaa na umaskini.

iv. Nyimbo za dini
Jitathmini 6.14 (ukurasa wa 38-39)

1. Nyimbo hizi huimbwa na waumini katika ibada.

2. Huimbwa kanisani au mahali popote ibada inapofanyika.

4.

- Hutumia lugha ya heshima kwa mfano uliyotenda maishani mwangu, mfalme wa amani.
- Huweza kuimbwa na mtu mmoja au kikundi cha watu. Wimbo huu umeimbwa na kikundi cha watu.
- Huwa na urudiaji mwingi. Wimbo huu una pambio.
- Hutumia lugha ya unyenyekevu: Moyo wangu na kinywa changu vitakuabudu daima.

5.

- Hutumiwa kumsifu Mungu. Kwa mfano: kizazi hadi kizazi kitajua wewe ni Mungu.
- Hutoa mafunzo kwa watu kuhusu imani. Kwa mfano: nilipokuwa mnyonge na dhaifu ulinipa nguvu mpya.
- Hutoa matumaini kwa watu wanaokumbwa na shida.

6. Wimbo huu unahusu mtu ambaye amepitia shida nyingi, watu wakamcheka na maadui wakafurahia ila sasa Mungu amemtendea makuu maishani mwake na hawezi kuusahau wema huo.

Lugha katika nyimbo

Jitathmini 6.15 (ukurasa wa 39)

1.

- Takriri
- Maswali ya balagha
- Sitiari
- Chuku
- Taswira
- Tashbihi

2.

- Takriri: hutumika kusisitiza ujumbe.
- Maswali ya balagha: hutumika kuwachochea wasikilizaji kujihoji na kutafakari kuhusu matendo yao.
- Sitiari: hutumika kulinganisha hali mbili bila kutumia viunganishi vya ulinganishaji.
- Chuku: husisitiza ujumbe unaopitishwa kwa kuutia chumvi ujumbe huo.
- Taswira: hutumia maelezo kumchorea mwimbaji au msikilizaji picha fulani akilini.
- Tashbihi: hutumika kulinganisha hali mbili kwa kutumia maneno ya ulinganishi kama vile *kama*, *mithili ya*.

3 (b)

- Sitiari: Pesa ni mbegu, Tamaa ni simba...
- Takriri: Pesa ni mbegu, lazima uipande...
- Taswira: Tamaa ni simba, anayenguruma sokoni,
  Ananiambia “nunua hiki”, ananivuta mwilini...
- Tashbihi: Lakini akili imesimama imara kama mwamba...
- Tashihisi: Tamaa ni simba, anayenguruma sokoni,
  Ananiambia “nunua hiki”, ananivuta mwilini...

(c)

- Sitiari: imetumika kulinganisha pesa na mbegu na kumchorea mwimbaji au msikilizaji picha akilini.
- Takriri: imetumika kusisitiza ujumbe kuhusu umuhimu wa kuwekezeza pesa ili izaane.
- Taswira: imetumika kumchorea mwimbaji na msikilizaji picha akilini na kumsaidia kuelewa ujumbe unaokusudiwa.
- Tashbihi: imetumika kuonyesha uwezo wa mtu kufanya uamuzi wa kuwekeza kwa kuepuka tamaa ya kuponda raha.
- Tashihisi: imetumika kuonyesha nguvu za tamaa katika maisha ya binadamu na juhudi zinazohitajika kuepuka hali hiyo.

(d) Tashihisi: Tamaa ni simba, anayenguruma sokoni,

Ananiambia “nunua hiki”, ananivuta mwilini...

Tashihisi hii imetumika kuonyesha nguvu za tamaa katika maisha ya binadamu na juhudi zinazohitajika kuepuka hali hiyo.

(e) Waimbie wenzako wimbo wowote.

(f) Hakiki hoja zako kwa kurejelea majibu ya zoezi la 2 katika shughuli hii.

4. Unaweza kutumia kipakatalishi, simu, tabuleti au kompyuta kufanya zoezi hili.

5. Fanya zoezi hili na mzazi au mlezi wako.

Wahusika katika nyimbo

Jitathmini 6.16 (ukurasa wa 40)

1. Wahusika hao wanaweza kuwa watu, wanyama au miungu.

2. (a) Ndugu yake Amina

(b) Amina, watoto wanaocheza

(c) Amina, Nduguye Amina

(d)

- Wakati wa kucheza mkikwaruzana msikasirikie haraka, hasira huleta chuki na kuongeza chuki.
- Tukikosana, ni vyema kuombana msamaha na kusameheana.

3. Unaweza kutumia kipakatalishi, simu, tabuleti au kompyuta kufanya zoezi hili. Tafiti tu kwenye mtandao salama kisha ufanye mazoezi uliyopewa.

4. Unapotunga wimbo na kumwasilishia mwenzako, hakikisha una wahusika wanyama ambao atawachanganua.

5. Fanya zoezi hili ukiwa na mzazi au mlezi wako. Hakikisha mnachanganua wahusika katika nyimbo hizo kwa kuangazia sifa zao.

d. Mazungumzo

i. Mawaidha

Jitathmini 6.17 (ukurasa wa 40-41)

2.

- Sifa za mawaidha ni kama vile:
- Hutumia lugha ya heshima.
- Huwa na ujumbe wa kufunza.
- Hutumia hoja na mifano kueleza ujumbe.
- Wahusika hubadilishana mawazo kwa utaratibu.
- Huwa na hitimisho lenye funzo.

3.

- Hukuza maadili.
- Husaidia kurekebisha tabia.
- Hujenga mshikamano wa watu katika jamii.
- Huelimisha vijana kuhusu maisha bora.

4 (a) Baba Musa anamshauri mwanawe Dhahabu ajenge mazoea ya kusoma ili afanikiwe masomoni jinsi alivyobobea katika mchezo.

(b) Mawaidha ya Baba Musa yanamwezesha Dhahabu kutambua kuwa bidii katika jambo lolote humsaidia mtu kufanikiwa katika jambo hilo.

(c) Hakuna jambo gumu maishani ikiwa mtu atatia juhudi katika jambo hilo.

ii. Malumbano ya utani

Jitathmini 6.18 (ukurasa wa 41-42)

1. Ni majibizano baina ya watu wawili au zaidi kwa njia ya mzaha.

2.

- Mjukuu na babu au nyanya.
- Ndugu na ndugu
- Wanarika
- Watu kutoka jamii mbili tofauti

3. (a) Kevo na Chacha; Ni marafiki na wanarika

(b) Kukosoa tabia hasi kama vile uvivu au uchoyo kwa njia ya ucheshi.

4. Kuwepo kwa uhusiano maalumu wa kiutani kati ya wanaohusika.